GOVERNMENT NOTICE No. 263 published on 31/3/2023

SHERIA YA USIMAMMIZI WA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI KWA MAGARI MATATU YA MRADI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO KAZI WA UFANISI WA NISHATI TANZANIA WA WIZARA YA NISHATI YA MWAKA 2023

Jinana kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi kwa Magari Matatu ya Mradi wa Mpango Kazi wa Ufanisi wa Nishati Tanzania wa Wizara ya Nishati ya Mwaka 2023 na itaanza kutumika kuanzia tarehe 22 Februari, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuimarishwa na Kamishna, kiasi chote cha kodi kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na magari yaliyoainishwa kwenye Jedwali, yanayoingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na kwaniaba ya Wizara ya Nishati, kwa ajili ya kutumiwa mahususi katika utekelezaji wa Mradi wa Mpango kazi wa Ufanisi wa Nishati Tanzania, kimesamehewa.

Masharti

3. Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba Amri hii haikutolewa, iwapo magari husika yatatumika kwa madhumuni tofauti au yatahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Kuisha kwa muda

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo tarehe 22 Agosti, 2023.

*Tangazo la Serikali Na. 263 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Maelezo | Idadi | Eneo la ununuzi Ndani ya Nchi/Nje ya Nchi |
|---|---|---|---|
| 1 | Land Cruiser 76 Hardtop 10seaters, 5 doors (A/C,ABS, Airbags, Power w/d, roof rack, HZJ76r-RKMRS-A3 Manual 2.8 GD-6(D-4D) | 01 | Nje ya nchi |
| 2 | Land Prado TXL, Turbo Diesel, 5door, 7-seater (Airbags, Climate Ctrl, ABS),GDJ150R-GKFEY-A1) | 02 | Nje ya nchi |

Dodoma,
17 Maci, 2023.

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha na Mipango*